

120

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA KUKODISHA GARI-FUSO 10 Tons KWA AJILI YA KUSAFIRISHA VIFAA VYA UJENZI-VIFAA VYA RANGI (PAINTING MATERIALS) KUTOKA DAR ES SALAAM KWENDA UTETE RUFUJI

KWA AJILI YA UJENZI WA CHUO CHA VETA RUFUJI

MKATABA NA: PA/024/2021/22/TRA/RUF/DVTC/01

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 16 mwezi 02 - 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha PWANI, S.L.P. 30345, KIBAHA, PWANI ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

M/S PASCHAL & SONS TRANSPORT COMMUSION AGENT wa S. L. P.70981 DAR ES SALAAM. (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni wa usafirishaji vifaa ") kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFUJI;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFUJI;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kazi za ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya RUFUJI ambayo ujenzi wake unaendelea;

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

### 1. GHARAMA ZA USAFIRISHAJI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 1,600,000/= kwa kuasafirisha vifaa vya ujenzi kutoka Dar es Salaam mpaka eneo la ujezi Utete Rufiji kama inavyoonekana kwenye jedwari hapo chini kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama “Gharama za usafirishaji vifaa vya ujenzi”

Gharama za kazi zitakazofanyika katika kila jengo ni kama ifuatavyo:

S/N	STAGE	BEI ILIYOKUBALIKA
1	GHARAMA ZITAKAZOTUMIKA KUSAFIRISHA VIFAA VYA RANGI KUTOKA KIWANDA CHA UZALISHAJI KIBOKO KWENDA DAR ES SALAAM MPAKA ENEO LA UJENZI UTETE RUFUJI. 9.5 Tons	1,600,000
	JUMLA	1,600,000

**2. MABADILIKO YA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI (TRANSPORTATION SUM ADJUSTMENT)**

Gharama za usafirishaji hazitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko yoyote yaliyofanywa na Mwajiri.

**3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO**

Malipo yatafanyika baada ya kazi kukamilika yaani Mzigo kufika eneo la ujenzi ukiwa salama na kwa idadi na kiwango kilichotakiwa.

**4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI**

(a) Mzabuni wa usafirishaji atakabidhi mzigo kwa wahusika wakuu waliopo eneo la ujenzi na kusainisha hati za mapokezi na nyaraka zingine muhimu kuonesha uhalali wa mapokezi ya mzigo husika.

(b) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Mzabuni wa usafirishaji kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo pasipo kuathiri pande zote.

**5. WAJIBU WA MZABUNI WA USAFIRISHAJI**

Mzabuni atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kusafirisha mzigo wa vifaa vya ujenzi kwa kadri alivyokubaliana katika mkataba sambamba na maelekezo ya Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA  
PWANI (PWANI RVTSC)

Jina: CLARA KUBONYA Saini: 


Wadhifa: AG PRINAPAL Tarehe: 16/02/2022

Mbele ya (Shahidi)


Jina: LUKA C. MKINI Saini: ~~\_\_\_\_\_~~

Wadhifa: MKITI KAMATI Tarehe: 16/02/2022  
YA USENZI

IMESAINIWA NA MZABUNI WA USAFIRISHAJI

Jina: PASCHAL RAINA Mbele ya   
Saini: \_\_\_\_\_  
Wadhifa: DIRECTOR Tarehe: 16/02/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: JULIUS JONAS Saini: 

Wadhifa: SECRETARY Tarehe: 16/02/2022

